# HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

# MUHTASARI NAMBA 2 WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UTAWALA NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 17/11/2021

**WAH. WALIOHUDHURIA:-**

1. Mh. Wilbard J. Bambara - Mwenyekiti
2. Mh. Andronizi E. Burindoli - Makamu Mwenyekiti
3. Mh. Mkubila S. Soud - Mjumbe
4. Mh. Mukiza Byamungu - Mjumbe
5. Mh. James E. Bazitsa - Mjumbe
6. Mh. Kened S. Festo - Mjumbe
7. Mh. Editha Mwinula - Mjumbe
8. Mh. Erick E. Nkilamachumu - Mjumbe
9. Mh. Catherine E. Maguru - Mjumbe
10. Bw. Solomon. O. Kimilike - Katibu

**Wajumbe wasiohudhuria- Kwa taarifa**

1. Mh. Mb. Ndaisaba Ruhoro (MB) - Mjumbe

**Wataalam waliohudhuria:**

1. Egidy Teulas - Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala
2. Bw. Yona Charugamba - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
3. Constantine F. Msemwa - Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji.
4. Oswald Rujuba - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
5. Didmus Bamuhiga - Kaimu Mratibu wa LADP
6. Adelina Mapunda -Kaimu Afisa Biashara
7. Eustach Ntayandi - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA
8. Ng'habi M. Mponeja -Mhasibu wa Mapato
9. Zacharia Mkumbo -Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
10. Enock Mponzi -Mkuu wa Idara ya Ardhi
11. Athanasio Andrew - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira
12. Joseph J. Mrianga - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Utalii
13. Emmanuel Kulwa -Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
14. Simon Mtuka -Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi
15. Asante Karara - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi
16. Cons tantine Mudende -Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo/ ushirika
17. Julius Bukobero -TEO –NGARA Mjini
18. Josephat Sangatati - Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
19. Sakina Y. Chamiti - Mratibu wa TASAF
20. Selialisi Antony -TEO-Rulenge
21. Dr. David S. Mapunda -Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
22. Singsbert Themistocles - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi
23. Bw. Jamary Idrisa - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi

**Miradi Mingine ya Maendeleo**

Halmashauri imepanga kutumia kiasi cha Tshs 8,763,358,200 kwa ajili ya miradi ya maendeleo nje ya Elimu bila malipo na miradi kutokana na Mapato ya ndani. Kwa mwezi Oktoba 2021 tumetumia kiasi cha Tshs 346,958,550 kwenye miradi ya maendeleo. Hivyo kuanzia Julai 2021 hadi kufikia Oktoba 2021 kiasi cha Tshs 412,863,450 kimetumika sawa na 32% ya bajeti ya mwaka.
Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili kama ifuatavyo;

Mwenyekiti alipongeza Menejimenti kwa kununua mashine za kukusanyia mapato (POS) za kutosha na kushauri Mkurugenzi na Mweka Hazina wafuatilie ukusanyaji wa mapato ili kuwepo na ufanisi.

Pia alisisitiza manunuzi yanayofanyika yazingatie sheria za manunuzi mikataba ya DRDP iandaliwe na baada ya kikao wajumbe wote watembelee mradi huo.

Aidha wajumbe walishauri kuwa Mganga Mkuu kufuatilia vitendo vinavyofanyika vituoni ili kusaidia makundi maalumu yanayotakiwa kupata huduma za matibabu bure na kushughulikia malalamiko yaliyoko huko.
Wajumbe waliipitisha taarifa

**AGENDA NA.16/MUHT.2/11/2021/2022:MAPENDEKEZO YA KUFANYA UHAMISHO WA NDANI WA VIFUNGU VYA MALIPO YA FEDHA ZITOKANAZO NA MAPATO YA NDANI KIASI CHA TSH. 183,594,505.00**

Iliwasilishwa taarifa ya mapendekezo ya uhamisho wa fedha Tshs. 183,594,505.00 ili ziweze kutekeleza miradi iliyoorodheshwa katika taarifa na miradi hiyo ianze kutekelezwa mara moja wakati taratibu zingine za kibajeti zinaendelea kufanyika baada ya kukamilika kwa nusu Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Wajumbe walishauri kwamba ni vyema wakaipitia taarifa hiyo kabla ya kwenda kwenye ziara ya ukaguzi wa mali za Halmashauri tarehe 25/11/2021.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI KUPITIA FEDHA ZA UVIKO 19**

Iliwasilishwa kwamba Halmashauri ya Ngara ilitengewa fedha kiasi cha **TShs. 2,710,000,000.00**kwa ajili ya miradi ya Afya, Elimu Msingi na Sekondari, ambapo kiasi

cha Tshs. **2,320,000,000.00** kimewekwa katika akaunti za shule na **Tshs. 390,000,000.00** zimewekwa katika akaunti ya Maendeleo ya Halmashauri.

Pamoja na maelekezo mengine Halmashauri ya Ngara ilielekezwa kufanya yafuatayo

i. Kuhakikisha utekelezaji wa miradi unaanza baada ya wiki mbili baada ya kupokea fedha.
ii. Kuhakikisha ujenzi wa madadasa unakamilika kabla au ifikapo **Desemba 15, 2021.**
iii. Vyumba vya madarasa vitakavyojengwa vijumuishe ununuzi wa seti 50 za meza na viti kwa shule za sekondari na madawati 15 kwa kila darasa katika vituo shikizi.
iv. Halmashauri kufanya manunuzi ya pamoja (*Bulk Procurement*) hasa kwa vifaa vya viwandani au kwa mawakala ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi.
v. Kuzingatia taratibu zote za matumizi ya fedha na kusimamia ubora wa ujenzi wa miundombinu kwa kutumia mfumo wa *Force Account.*

**Pamoja na maelekezo ya utekelezaji wa mradi huo mambo yafuatayo yalifanyika ngazi ya Halmashauri kwa kushirikina na Wasimamizi walioko katika maeneo yenye miradi**

- Vifaa vyote vya viwandani vitanunuliwa na Makao Makuu ya Halmashauri.
- Vifaa vinavyopatikana maeneo ya mradi (tofali, mawe na mchanga n.k) vitaendelea kununuliwa kwenye maeneo ya mradi baada ya Kamati ya usimamizi ya Miradi Ngazi ya Halmashauri baada ya kupitia na kujiridhisha ili kudhibiti matumizi makubwa yasiyo ya lazima.
- Mafundi wote walipatikana na wanaendelea kufanya kazi kwa bei elekezi isiyozidi TSh.2,300,000/= isipokuwa maeneo yenye miteremko mikali
- Kibali cha kubadili maeneo ya mradi kwa vituo shikizi kilitolewa na ujenzi unaendelea.
- Taratibu za kupanua vifungu vya malipo kwa ajili ya TShs. 390,000,000.00 za Sekta ya Afya zinaendelea kwani fedha hizo ziliwekwa katika akaunti za Vituo vya Afya

Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili kama ifuatavyo;

Wajumbe walishauri kwamba kabla ya kutembelea mali za Halmashauri wapitie taarifa ya mapendekezo ya kufanya uhamisho wa ndani wa vifungu vya malipo ya fedha zitokanazo na mapato ya ndani kiasi cha tsh. 183,594,505.00 ili kubaini kama fedha itakayohamishwa hazitaathiri maboma ya maeneo gani ili wahuka walijue suala hilo vizuri.

**Azimio:** Wajumbe waliazimia kwamba tarehe kabla ya kutembelea mali za Halmashauri wapitie taarifa ya mapendekezo ya kufanya uhamisho wa ndani wa vifungu vya malipo ya fedha zitokanazo na mapato ya ndani kiasi cha Tsh. 183,594,505.00, na baada ya ziara hiyo wajumbe watafanya majumuisho.

x) Ukarabati wa barabara kiwango cha changarawe Kutoka barabara kuu kwenda kituo cha afya Rusumo

Mratibu wa LADP alitoa taarifa kuwa wapo wananchi wachache ambao hawakuridhia kutoa maeneo yao na wajumbe wakaazimia kutembelea maeneo hayo ili kuhamasisha maendeleo.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili kama ifuatavyo;
Iliazimiwa kwamba kwamba wananchi ambao hawakuridhia kutoa maeneo yao iundwe timu ya kuwafuatilia na kuwaelimisha ili waweze kutoa maeneo yao.
**Azimio:** Iliazimiwa kuwa wananchi ambao hawakuridhia kutoa maeneo yao iundwe timu ya kuwafuatilia na kuwaelimisha ili waweze kutoa maeneo yao.

**AGENDA NA.20/MUHT NA 11/ 10/2021/2022: KUFUNGA KIKAO**
Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na kikao kilifungwa rasmi saa 09.30 alasiri.

***UMETHIBITISHWA NA;***

.................................... ....................................
**Katibu** **Mwenyekiti**

**Taraehe**....20../..12......**/2021**